


# "MWANA NDIYE MFANO WETU WA UNYENYEKEVU"

Hujambo!

Nakusalimu hujambo asubuhi ya leo.

Tunaendeleza ugunduzi wetu wa Yesu-Aliye ama Yesu Halisi katika Wafilipi 2:5-11:

> **WAFILIPI 2:5** *'Muwe na msimamo uleule aliokuwa nao Kristo Yesu: Yeye, kwa asili alikuwa daima Mungu; lakini hakufikiri kwamba kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kungangania kwa nguvu. Bali, kwa hiari yake mwenyewe, aliachilia hayo yote, akajitwalia hali ya mtumishi, akawa sawa na wanadamu, akaonekana kama wanadamu.'*

Mwana alikuwa na anazo sifa zote za Baba. Yeye ni;

- Mwenye nguvu zote
- Anayejua vitu vyote, na
- Aliye kila mahali.

Lakini, ili kutimiza kusudi la Mungu duniani – uumbaji wa Watu wa kipekee wanaoitwa kwa jina lake ambao anakuja kukaa ndani yao sasa na hata milele – Mwana hakufanya hivyo akikusudia kuwa sawa na Baba. Badala yake aliweka kando sifa zake tatu za Kiungu ili "kujimwaga" ndani ya Yesu wa Nazareti.

> **WAFILIPI 2:8** *Naye alipoonekana ana sura kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti; hata kifo msalabani*

Je, kuna kitu cha kushangaza zaidi kuliko hiki?

Kwamba Mungu katika Mwana wake angejinyenyekeza ili ahukumiwe bila haki, ateswe kikatili, na Kusulubiwa hadi kufa uchi mbele ya umati mkubwa wa sikukuu ya Pasaka huko Yerusalemu?

Fikiria hili: mwandishi wa maisha kwa hiari alijitoa kwenye kifo cha kutisha, cha aibu ili sisi sote tuwe huru kutoka kwa;

- Nguvu ya dhambi – 1 Wakorintho 15:56; Wakolosai 2:14
- Hatia ya dhambi zetu – Isaya 53:1-12
- Aibu ya dhambi zetu – 1 Petro 2:6
- Laana ya Sheria – Wagalatia 3:13
- Nguvu za Shetani – Wakolosai 2:15, na
- Nguvu ya kifo. – Waebrania 2:13b-14; Warumi 5:17; Warumi 6:23

Alifanya mambo haya yote kwa ajili yenu, kwa ajili yako na yangu – kwa kila mtu anayetoa maisha yake kwa Kristo Yesu.

> **WAFILIPI 2:9-11** *'Kwa sababu hiyo Mungu alimkweza juu kabisa, akampa jina lililo kuu kuliko majina yote. Ili kwa heshima ya jina la Yesu, viumbe vyote mbinguni, duniani na kuzimu, vipige magoti mbele yake, na kila mtu akiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.'*

Leo, Yesu ameketi mbinguni kwenye mkono wa kuume wa Baba anayetawala ulimwengu na maisha yote yaliyo duniani.

Na zaidi ya hayo, inakuja Siku ya Bwana, wakati Yesu atakapotokea mbinguni kama Amiri wa Majeshi ya Malaika akiwasili kuwatupa waovu katika jehanamu ya moto na kukusanya watu wake na kuanzilisha Utawala wa Mungu duniani kwa miaka elfu moja.

Na siku hiyo kila kiumbe, kilicho hai na kilicho kufa, marafiki na maadui zake, malaika na mapepo – watapiga magoti na kumtukuza Mungu kwa kupiga kelele ya Ukweli wa milele: Yesu ni Bwana!

Nakuuliza:
- Je, umetoa maisha yako kabisa kwa huyu Yesu-Aliye yaani Yesu Halisi?
- Je, umepata kusudi lako maishani kwa kumpenda na kumtumikia huyu Yesu-Aliye yaani Yesu Halisi?
- Je, umekuwa ukihubiri na kushiriki na kila mtu huyu Yesu-Aliye yaani Yesu Halisi?

Basi umshikilie sana na zaidi. Usiondoe macho yako kwake. Usiangalie nyuma kamwe. Maliza ulichoanza katika Yesu-Aliye yaani Yesu Halisi.

Hivi karibuni ataonekana, atakukuleta karibu na yeye mwenyewe na atakukaribisha katika umilele.

Na mpaka wakati huo, utaushinda ulimwengu, mwili wako, na pia utamshinda shetani kwa uwezo wa damu ya Yesu Kristo pamoja na ushuhuda wako.

Kila mtu amealikwa. Kila mtu anaalikwa bila kuchelewa. Kila mtu amealikwa milele.

WIKI IJAYO: Zaidi kuhusu Yesu-Aliye – Yesu sahihi, Yesu kamili.

Pokea baraka kwa jina la Yesu.



Douglas Van Devender.
Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.

**TANGAZO LA KUZINGATIA:**
Wengine wanaweza kuongezwa kwenye orodha yetu ya barua-pepe kwa kutuma majina yao, eneo na barua pepe kwa [WDV2023@outlook.com](mailto:WDV2023@outlook.com)
(Mtu yeyote anaweza kujiondoa kwa kutuma neno STOP kwa anwani sawa ya barua pepe.) Ahsante.